

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

47. Akasema: "Mtalima myaka saba mfululizo kwa juhudi (yaani limeni miaka saba kwa juhudi kwani itaingia njaa kubwa baada ya myaka saba). Na mtakavyovivuna viacheni katika mashuke yake, isipokuwa kidogo mnavyokula (ili hivyo mnavyoviacha mule katika myaka ya njaa itakayokuja)."

48. "Kisha itakuja baadaye myaka saba ya shida itakayokula vile mlivyoipa, (yaani watu watakula ile akiba mliyoiweka) isipokuwa kidogo mtakachohifadhi (kwa ajili ya kupandia)."

49. "Kisha baada ya haya utakuja mwaka ambao katika mwaka huo watu watasaidiwa na (Mwenyezi Mungu); na katika huo watakamua (vya kukamua)."

50. Na mfalme (alipopelekewa khabari hii) alisema: "Mleteni kwangu." Basi mjumbe (wa mfalme) alipomjia (Yusufu, alisema Yusufu) "Rudi kwa bwana wako ukamuulize khabari ya wanawake wale waliokata mikono yao; bila shaka Mola wangu anazijua sana hila zao (lakini nataka mfalme ajue usafi wangu ili anitakasie nia, asiniogope)."

51. (Mfalme akawakusanya wale wanawake na akasema): "Nini jambo lenu lilikuwa mlipomtamani Yusufu kinyume cha matamania yake?" Wakasema: "Hasha lillahi! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake (Tumejitahidi afanye mabaya na sisi, hakukubali kufanya)." Mkewe waziri (naye) akasema: "Sasa haki imedhihirika, mimi ndiye niliyemtamani kinyume cha nafsi yake, na bila shaka yeye yu miongoni mwa wakweli (kabisa)."

52. (Na Yusufu akasema): "Hayo (ya kutaka waulizwe hivi) ni kwa sababu (waziri) ajue ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana nyuma yake; na ya kwamba Mwenyezi Mungu hazijaalii hila za makhaini kufanikiwa."

53. Nami sijitakasi nafsi yangu; kwa hakika (kila) nafsi ni yenye kuamrisha sana maovu, isipokuwa ile ambayo Mola wangu ameirehemu. Hakika Mola wangu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَابَّاءَ فَمَا حَصَدْتُمْ
فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلِهِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾

ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ سَبْعٌ شِدَادٌ يَأْكُلْنَ
مَا قَدَّمْتُمْ لَهُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَحْصُونَ ﴿٤٨﴾

ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَامٌ فِيهِ يُغَاثُ النَّاسُ وَ
فِيهِ يَعْصَرُونَ ﴿٤٩﴾

وَقَالَ الْمَلِكُ ائْتُونِي بِهِ : فَلَمَّا جَاءَهُ الرَّسُولُ
قَالَ ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَعَلَّهُ مَا بَالَ النِّسْوَةِ الَّتِي
قَطَعْنَ أَيْدِيَهُنَّ إِنَّ رَبِّي بِكَيْدِهِنَّ عَلِيمٌ ﴿٥٠﴾

قَالَ مَا خَطْبُكَ إِذْ رَأَوْنِي يُوسُفَ عَنْ نَفْسِهِ
قُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ قَالَتِ امْرَأَتُ
الْعَزِيزِ الَّتِي حَصَصَ الْحَيُّ أَنْارَاوْدَتُهُ عَنْ نَفْسِهِ
وَإِنَّهُ لَكِنَّ الصَّادِقِينَ ﴿٥١﴾

ذَلِكَ لِيَعْلَمَ أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ بِالْغَيْبِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي
كَيْدَ الْخَائِنِينَ ﴿٥٢﴾

وَمَا أُبَرِّئُ نَفْسِي إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ
بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٣﴾

47. Hakumkasirikia akamwambia sikwambii usije ukapata ukubwa usiostahiki.

53. Ingawa inapasa mtu kukitakasa cheo chake lakini haipendezi kujisifu. Basi ndiyo hapa anabainisha kuwa haya aliyoyataka kwa mfalme ni kwa ajili ya kujitakasa asionekane kuwa mbaya na mwizi wa fadhila, sio kwa ajili ya kutaka kujionesha. Tarumbeta la kujipigia mtu mwenyewe halipendezi.

Na kule kujisifu kwake Nabii Yusufu katika Aya ya 55 ni kwa ajili ya dharura. Kwa ajili apewe yeye kazi ya

54. Basi mfalme akasema: "Mleteni kwangu, nimchague awe mtu wangu mwenyewe." Basi alipozungumza naye (mfalme) alisema, "Hakika wewe leo kwetu umekwishakuwa ni mwenye hishima na muaminiwa."

55. Akasema (Yusufu): "Nifanye mtazamaji wa khazina za nchi (yote); hakika mimi ni Mlinzi mzuri na mjuzi hodari."

56. Basi namna hivi tukampa Yusufu cheo katika nchi hiyo (ya Misri); anakaa humo popote anapopenda. Tunamfikishia rehema zetu tumtakaye, wala hatupuzi malipo ya wafanyao mema.

57. Na bila shaka malipo ya Akhera ni bora zaidi, kwa wale walioamini na wakawa wanaogopa.

58. Wakaja ndugu zake Yusufu (kutaka chakula katika nchi kama walivyokuwa wakija watu wa nchi nyingine huko kwani njaa ilikuwa imekwishaingia Mashariki ya Kati yote nzima) na wakaingia kwake; akawajua, (lakini) wao hawakumjua.

59. Na alipowapatia chakula chao alisema: "(Mkinijia mara ya pili) nijieni na ndugu yenu wa kwa baba. Je! Hamuoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo, nami ni mbora wa wakaribishao? (Basi nitakukaribisheni nyote kwa uzuri)."

60. "Na kama hamtaniletea, basi hamtakuwa na kipimo (cha chakula) chochote kwangu, wala msinikurubie."

61. Wakasema: "Sisi tutamrairai baba yake (mpaka atupe); na bila shaka tutafanya haya."

62. Na (Yusufu) akawaambia watumishi wake; "Mali yao (waliyoleta kubadilisha na chakula) yatieni katika mizigo yao, ili wayaone watakaporudi kwa watu wa nyumbani kwao; (tukifanya hivi) huenda watarejea."

63. Basi waliporejea kwa baba yao, walisema: "Ewe baba yetu! Tutazuiliwa (chakula mara ya pili

وَقَالَ الْمَلِكُ اَتُونِي بِهِ اَسْتَخَصُّهُ لِنَفْسِي، فَلَمَّا كَلَّمَهُ قَالَ اِنَّكَ الْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِينٌ اَمِينٌ ⑤

قَالَ اجْعَلْنِي عَلَى خَزَائِنِ الْاَرْضِ اِنِّي خَفِيفٌ عَلَيْهِمْ ⑥

وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْاَرْضِ، يَتَّبِعُوهُ مِنْهَا حَيْثُ شَاءَ، وَنُصِيبُ بِرَحْمَتِنَا مَنْ نَشَاءُ وَلَا نُضِيعُ اَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ⑦

وَلَا جُرْاَ الْاِخْرَجُوْا خَيْرٌ لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَكَانُوْا يَتَّقُوْنَ ⑧

وَجَاءَ اِخْوَةُ يُوْسُفَ فَدَخَلُوْا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُ مُنْكَرُوْنَ ⑨

وَلَمَّا جَهَّزَهُمْ بِجَهَازِهِمْ قَالَ اِتُونِي بِاَخِيْ لَكُمْ مِّنْ اَبْنِكُمْ اَلَا تَرَوْنَ اَنِّيْ اُوْفِي الْكَيْلَ وَاَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِيْنَ ⑩

قَالَ لَمَّا رَاْتُوْنِيْ بِهِ فَلَا كَيْلَ لَكُمْ عِنْدِيْ وَلَا تَقْرَبُوْنِ ⑪

قَالُوْا سَرَاوُدُ عَلَيْهِ اَبَاةٌ وَاِنَّا لَفَاعِلُوْنَ ⑫

وَقَالَ لِفَتَاتِهِ اجْعَلُوْا بِضَاعَهُمْ فِيْ رِحَالِهِمْ لَعَلَّهُمْ يُرْجَوْنَ اِذَا اُنْقَلَبُوْا اِلَى اَهْلِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ⑬

فَلَمَّا رَجَعُوْا اِلَى اَبِيْهِمْ قَالُوْا يَا اَبَانَا مُنِعَ مِنَّا

kutazama kinachoingia na kutoka ili akigawe vizuri; kila mtu asikose, la katika nchi hiyo wala nchi zilizo karibu yao wakati itakapoingia njaa. Alikuwa na yakini kuwa hakuna atakayeweza kuyafanya hayo ila yeye.

Basi na mwengine yoyote ni vile vile, akijiona yeye ndiye anayeweza kuliendesha vilivyo jambo hilo naalitake, lakini asilitake asiloliweza. Akifanya hivyo atakuwa anajidhulumu yeye na anadhulumu wenziwe na anadhulumu uma.

55. Basi akapewa cheo cha kuwa Khazina yote iwe chini ya mikono yake. Basi akajenga maghala mengi sana sana na akawa ananunua ghila (nafaka) anajaza tele tele humo ili zije nafaka hizo zifae Mashariki ya Kati yote nzima wakati itakapoingia njaa kote humo. Basi muda wa myaka saba akawa anajazajaza tu.

mpaka twende na ndugu yetu); basi mpeleke ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa; na yakini sisi tutamlinda.”

64. Akasema: “Ndiyo nikuaminini juu ya huyu kwa namna nyingine) isiyokuwa kama vile nilivyokuaminini juu ya nduguye zamani (mkampoteza)? Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa kulinda, naye ndiye anayerehemu kweli kweli kuliko wenye kurehemu wote.”

65. Na walipofungua vitu vyao, wakakuta mali zao zimerudishwa kwao, walisema: “Ewe baba yetu! Tunataka kingine nini (tena kwa mtu huyu?) Hii mali yetu imerudishwa kwetu! Na tumeleta chakula kwa ajili ya watu wetu, na tutamlinda ndugu yetu, na tutapata kipimio cha ngamia mmoja zaidi; hicho ni kipimo kidogo (kwa huyo mfalme, hataona uzito kutupa).”

66. Akasema: “Sitampeleka pamoja nanyi mpaka munipe ahadi kwa jina la Mwenyezi Mungu ya kwamba lazima mtamrejea kwangu, isipokuwa mzungukwe nyote (na khatari au kufa).” Basi walipompa ahadi yao alisema: “Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi (Shahidi) juu ya haya tusemayo.”

67. Na akasema: “Enyi wanangu! Msiingie (Misri) katika mlango mmoja, bali ingieni katika milango mbalimbali; wala sikufaeni chochote mbele (qadhaa) ya Mwenyezi Mungu. Hukumu haiko ila kwa Mwenyezi Mungu tu. Kwake nimetegemea, na wategemeao nawategemee kwake.”

68. Na walipoingia jinsi alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa haja iliyokuwa katika nafsi ya Yaaqubu aliitimiza (Alikuwa akitaka asadifiane na Yusufu — ndugu yake yule khalisa, peke yao. Wakasadifiana hivyo). Na bila shaka yeye (Yaaqubu) alikuwa mwenye ilimu kwa sababu tulimfundisha, lakini watu wengi hawajui.

69. Na walipoingia kwa Yusufu (akamuona ndugu yake na alikuwa ameingia peke yake) alimkumbatia huyo ndugu yake akasema: “Hakika mimi ni ndugu yako. Basi usihuzunike kwa sababu ya yale waliyokuwa (ndugu zetu) wakifanya (na

الرَّكِيْلَ فَأَرْسَلْ مَعَنَا أَخَانَا نَكْتَلْ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٦٤﴾

قَالَ هَلْ أُمِنُكُمْ عَلَيْهِ إِلَّا كَمَا أُمِنْتُكُمْ عَلَيْهِ إِجِبْهُ مِنْ قَبْلُ ۚ قَالَ خَيْرٌ حَافِظًا وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٦٥﴾

وَلَمَّا فَتَحُوا مَتَاعَهُمْ وَجَدُوا بِضَاعَتَهُمْ رُدَّتْ إِلَيْهِمْ ۚ قَالُوا يَا أَبَانَا مَا نَبْغِي هَذِهِ بِضَاعَتُنَا رُدَّتْ إِلَيْنَا وَنَبِئْ أَهْلَنَا وَنَحْفَظْ أَخَانَنَا وَنَزِدَادُ كَيْلَ بَعِيرٍ ذَلِكَ كَيْلٌ يَسِيرٌ ﴿٦٦﴾

قَالَ لَنْ أَرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُتَوَّنَ مَوْتًا مِّنَ اللَّهِ ۚ كَتَبْتُ نَتَّبِعِي بِهِ إِلَّا أَنْ يُحَاطَ بِكُمْ فَلَمَّا اتَّوَتْ مَوْتَهُمْ قَالَ اللَّهُ عَلَى مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٦٧﴾

وَقَالَ يَبْنَئِي لَا تَدْخُلُوا مِنِّي بَابَ وَاحِدٍ وَّادْخُلُوا مِن أَبْوَابٍ مُّتَفَرِّقَةٍ ۚ وَمَا أُغْنِي عَنْكُمْ مِّنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٦٨﴾

وَلَمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ ۚ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا حَاجَةً فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَاهَا ۚ وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لِّمَا عَلَّمْنَاهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٩﴾

وَلَمَّا دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ أَوَّعَ إِلَيْهِ أَخَاهُ قَالَ إِنِّي أَنَا أَخُوكَ فَلَا تَبْتَئِسْ

67. Inasemekana ya kuwa huyu baba yao (Nabii Yaaqubu) alikuwa akihiisi kuwa huyo mkubwa aliyoko Misri aliyewafanyia hayo na akataka haya ni mwanawe—Nabii Yusufu. Akataka apate fursa huyo mwanawe anayekwenda sasa akutane na huyo nduguye peke yao ambaye ndiye nduguye khalisa. Hawa kumi waliosalia walikuwa wa mama mbali mbali.

nitakayokufanyia hila ili nipate kukuzuia hapa unieleleze habari za kwetu.”

70. Na alipokwishawapatia chakula chao, akaweka jagi (gudulia) la kunywea maji katika mzigo wa nduguye huyo, kisha mnadi akanadi: “Enyi wasafiri! Hakika nyinyi ni wezi.”

71. (Wote wale ndugu zake Yusufu), na hali ya kuwa wamewaelekea (wale wanaonadi), walisema “Kwani mumepoteza nini (hata mnasema kuwa sisi ni wezi)?”

72. Wakasema: “Tumepoteza pishi ya mfalme (wanayopimiwa watu ambayo asili yake ilikuwa gudulia); na atakayeileta atapewa mzigo wa ngamia,” na (Nabii Yusufu akasema): “Nami ni dhamini juu ya haya.”

73. Wakasema: “Wallahi! Mumekwishajua (tangu tulipokuja mara ya kwanza) ya kwamba sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi (yenu hii), wala sisi si wezi.”

74. Wakasema: “Basi malipo yake yatakuwa nini kama nyinyi mnasema uwongo?”

75. Wakasema: “Malipo yake ni yule ambaye itaonekana (pishi hiyo) katika mzigo wake; basi yeye ndiye malipo yake (atafanywa mtumwa kwenu muda wa mwaka mzima). Hivi ndivyo tunavyowalipa madhalimu.”

76. Basi akaanza (Nabii Yusufu) katika mizigo yao kabla ya mzigo wa nduguye; kisha akaitoa katika

بَنَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٠﴾

فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِجَهَارِهِمْ جَعَلَ السَّقَايَةُ فِي رَحْلِ أَخِيهِ ثُمَّ أَذَّنْ مُؤَذِّنٌ أَيُّهَا الْعِبْرُ إِنَّكُمْ لَسِرْقُونَ ﴿٧١﴾

قَالُوا وَاقْبَلُوا عَلَيْهِمْ مَاذَا تَفْقَدُونَ ﴿٧٢﴾

قَالُوا نَفْقَدُ صَوَاءَ الْمَلِكِ وَلِمَنْ جَاءَ بِهِ حِمْلُ بَعِيرٍ وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ ﴿٧٣﴾

قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا جِئْتَنَا لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كُنَّا سَارِقِينَ ﴿٧٤﴾

قَالُوا فَمَا جَزَاؤُهُ إِنْ كُنْتُمْ كَذِبِينَ ﴿٧٥﴾

قَالُوا جَزَاؤُهُ مَنْ وُجِدَ فِي رَحْلِهِ فَهُوَ جَزَاؤُهُ كَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٧٦﴾

فَبَدَأَ بِأَوْعِيَّتِهِمْ قَبْلَ رَعَاءِ أَخِيهِ ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا

70. Anafanya ujanja wa kumzuia apate kuzungumza naye yote yaliyopita tangu alipotolewa huko na nduguze.

70, 72. Aya hizi walizozifanya ni za 71 na 73 wameipindua tafsiri ya Jaala wakadai ina maana mbili. Maana yake ni hiyo hiyo moja tu; kuwa amefanya hivyo kusudi ili apate njia ya kumzuia yule khalisa wake (ndugu yake baba mmoja mama mmoja) ili amzungumze mbele — kabla hajakutana na wazee wake na jamaa zake — yaliyopita tangu kuondoka kwake. Wala hakuna mfasiri yoyote aliyemlaumu Nabii Yusufu. Atamlaumu bila ya kustahiki kulaumiwa? Waongo tu basi. Na wanadai *Suwaa* mbali na *Siqaya*, na hali ya kuwa ndicho hicho hicho kitu kimoja—kikifanya kazi mbili. Kwani karasia inayotumiwa kwa kupimia maziwa haitumiwi kwa kunywea maji? Au sinia inayotumiwa kwa kulia chakula haitumiwi kwa kukandia? Wanajua Wanajitia Hamnazo kusudi, Wakacheza Ngoma Watakazo. Na ngoma hizo zote makusudio yake kuwapoteza Waislamu.

Na wakasema kuwa tamko la *Kidnaa* iliyoko katika Aya waliyoifanya kuwa ni ya 77, linaonyesha kuwa hayo hayakupangwa na Nabii Yusufu, lakini yametokea tu kwa mipango ya Mwenyezi Mungu bila kudhani Nabii Yusufu kuwa yatatokea hayo. Tunasema — kama wanavyosema wafasiri wote — kuwa yametokea haya kwa mpango wa Nabii Yusufu kwa Wahyi alioletewa na Mwenyezi Mungu kuwa afanye VILE, itakuwa HIVYO. Wasitutilie uvugu katika dini yetu.

75. Ilikuwa katika Sharia yao mwizi anafanywa mtumwa wa yule aliyemuibia.

76. Inaonyesha kuwa wenye ilimu huyafikilia wayataayo kwa njia nzuri. Na kila ukipata ilimu, taka zaidi.

mzigo wa nduguye. Hivi ndivyo tulivyomfanyia hila Yusufu (ya kuweza kumpata nduguye). Hakuweza kumzuia nduguye kwa kanuni ya mfalme (wa nchi ile; siyo hukumu yao hii); isipokuwa alivyotaka Mwenyezi Mungu (basi wale nduguze walitaja hukumu ya kwao ya kumfanya mtumwa mtu anayeiba). Tunawainua katika vyeo (vikubwa) wale tuwatakao; na juu ya kila ajuaye yuko ajuaye zaidi.

77. Wakasema: “Kama ameiba, basi ndugu yake pia aliiba zamani” (wanamsingizia uwongo Nabii Yusufu, wala hawana khabari kuwa huyu aliye mbele yao ndiye Nabii Yusufu). Lakini Nabii Yusufu akayaficha moyoni mwake wala hakuwadhihirishia. Akasema: “Nyinyi muna hali mbaya (zaidi kuliko huyo); na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyasema.”

78. Wakasema: “Ewe bwana! Huyu anaye baba mzee sana, kwa hivyo mchukue mmoja wetu badala yake; bila shaka sisi tunakuona umo miongoni mwa wafanyao ihsani (kubwa).”

79. (Yusufu) akasema: “Mungu aepushe mbali Inshaallah kumkamata isipokuwa yule tuliyeyakuta mali yetu yako kwake; tusije kuwa madhalimu.”

80. Basi walipokata tamaa naye, walikwenda kando kunong'ona. Mkubwa wao akasema: “Je! Hamjui ya kwamba baba yenu amechukua ahadi juu yenu kwa jina la Mwenyezi Mungu (kuwa mtamrejeza huyo)? Na zamani pia mlikosa katika (maagano yenu juu ya) Yusufu! Basi sitaitoka nchi hii mpaka baba yangu anipe ruhusa au Mwenyezi Mungu anihukumie (la kuniondosha hapa). Naye ndiye mbora wa mahakimu.”

81. “Rudini kwa baba yenu, na semeni ‘Ee baba yetu! Mwanao ameiba: na sisi hatukutoa shahada ile (ya kuwa mwizi atekwe) isipokuwa kwa yale tuliyoyajua (ya kuwa hakuna mwizi katika sisi); na hatukuwa tunajua yaliyokuwa katika siri.’ (Sisi tulishuhudia kuwa kwetu anayeiba hufanywa mtumwa, wala hatukujua kuwa yeye ndiye aliyeiba).”

82. “Na waulize watu wa mji tuliokuwa, na (waulize watu wa) msafara tuliokuja nao; na hakika sisi tunasema kweli.”

مِنْ رَّعَايَ أَخِيهِ، كَذَلِكَ كِدْنَا لِيُوسُفَ مَا كَانَ لِيَأْخُذَ أَخَاهُ فِي دِينِ الْمَلِكِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ، نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مِمَّنْ نَشَاءُ، وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ ⑦

قَالُوا إِنْ يَسْرِقْ فَقَدْ سَرَقَ أَخٌ لَهُ مِنْ قَبْلُ، فَأَسْرَهَا يَوْسُفُ فِي نَفْسِهِ وَلَمْ يُبْدِهَا لَهُمْ، قَالَ أَنْتُمْ شَرُّ مَكَانٍ، وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ ⑧

قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ إِنَّ لَهُ أَبًا شَيْخًا كَبِيرًا فَخُذْ أَحَدًا مَكَانَهُ، إِنَّا نَرَاكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ⑨

قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ أَنْ نَأْخُذَ إِلَّا مَنْ وَجَدْنَا مَتَاعَنَا عِنْدَهُ، إِنَّا إِذَا الظَّالِمُونَ ⑩

فَلَمَّا اسْتَيْسَسُوا مِنْهُ خَلَصُوا نَجِيًّا، قَالَ كَبِيرُهُمْ أَلَمْ تَعْلَمُوا أَنَّ أَبَاكُمْ قَدْ أَخَذَ عَلَيْكُمْ مَوْثِقًا مِنَ اللَّهِ وَمِنْ قَبْلُ مَا كُنْتُمْ فِي يَدَيْ يَوْسُفَ، فَلَنْ أَبْرَحَ الْأَرْضَ حَتَّى يَأْذَنَ لِي أَوْ يَحْكُمَ اللَّهُ لِي، وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ⑪

ارْجِعُوا إِلَى آبَائِكُمْ فَقُولُوا يَا أَبَا نَا إِنَّ ابْنَكَ سَرَقَ، وَمَا شَهِدْنَا إِلَّا بِمَا عَلَّمَنَا وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ حَافِظِينَ ⑫

وَسَلَّ الْقَرْيَةَ الَّتِي كُنَّا فِيهَا وَالْعَيْرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فِيهَا، وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ⑬

79. Hakusema aliyeiba. Alisema 'tuliyeakuta mali yetu yako kwake' kwani kwa hakika yeye hakuiba. Inataka mtu akisema aseme kwa hadhari.

83. (Yaaqubu) akasema: "Bali nafsi zenu zimekuzainishieni kumfanyia jambo. (Langu mimi ni) subira njema. Hwenda Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja; bila shaka Yeye ni Mjuzi na Mwenye hikima."

84. Na akajitenga nao na akasema: "Oo! Majonzi yangu juu ya Yusufu!" Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni (Mboni zimefunikwa na weupe); Naye alikuwa amejaa (huzuni).

85. Wakasema: "Wallahi! Hutaacha kumkumbuka Yusufu (na kulia) hata utakuwa mgonjwa au utakuwa miongoni mwa wenye kuangamia."

86. Akasema: "Hakika mimi nashtakia sikitiko langu na huzuni yangu kwa Mwenyezi Mungu, (sikushitakieni nyinyi). Na najua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua.

87. "Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusufu na nduguye, wala msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri."

88. (Wakenda tena Misri). Basi walipoingia kwa (Yusufu), wakasema "Ewe bwana! Shida imetupata sisi na watu wetu, na tumeleta mali isiyotakiwa. Tupimie kipimio kamili (juu ya upungufu wa mali yetu) na utufanyie zile fadhila zako (za kila mara). Hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wanaowafanyia fadhila wenziwao."

89. Akasema: "Je! Mnajua mliyomfanyia Yusufu na ndugu yake mlipokuwa ujingani?"

90. Wakasema: "Je! Wewe ndiye Yusufu?" Akasema: "Mimi ndiye Yusufu, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu ametufanyia hisani. Hakika anayemcha Mungu na kusubiri (Mwenyezi Mungu humlipa). Hakika Mwenyezi Mungu hapuzi malipo ya wafanyao mema."

91. Wakasema: "Wallahi! Mwenyezi Mungu amekuchagua juu yetu, na hakika sisi tulikuwa wenye khatia (makosa)."

قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا فَصَبِّرْ
جَمِيلٌ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَنِي بِهِمْ جَمِيعًا
إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ٨٣

وَوَلَّى عَنْهُمْ وَقَالَ يَا سَفَى عَلَى يُونُسَ
وَأَبْصَحْتَ عَيْنُهُ مِنْ الْحُزَنِ فَهُوَ كَظِيمٌ ٨٤

قَالُوا تَاللَّهِ تَفْتَوْا تَذَكَّرُ يُونُسَ كَيْتُ تَكُونُ
حَرْصًا أَوْ تَكُونُ مِنَ الْهَالِكِينَ ٨٥

قَالَ إِنَّمَا أَشْكُوا بَثِّي وَحُزْنِي إِلَى اللَّهِ وَأَعْلَمُ مِنَ
اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ٨٦

يَذَرْنِي أَذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِنْ يُونُسَ وَأَخِيهِ وَلَا
تَأْتِيَهُمْ رَوْحُ اللَّهِ إِنَّهُ لَا يَأْتِيَنَّ مِنْ رَوْحِ
اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمَ الْكَافِرُونَ ٨٧

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَيْهِ قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ مَسَّنَا
وَأَهْلْنَا الضَّرُّ وَجِئْنَا بِبِضَاعَةٍ مُرْجَاةٍ فَأَوْفِ لَنَا
الْكَيْلَ وَ تَصَدَّقْ عَلَيْنَا إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي
الْمُتَصَدِّقِينَ ٨٨

قَالَ هَلْ عَلِمْتُمْ مَا فَعَلْتُمْ يُونُسَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنْتُمْ
جَاهِلُونَ ٨٩

قَالُوا أَمْ إِنَّا لَأَنْتَ يُونُسَ قَالَ أَنَا يُونُسَ
وَهَذَا أَخِي فَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا إِنَّهُ مَنْ
يَشَاءُ يَصْطَرِّقُ اللَّهُ لَا يُضَيِّعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ٩٠

قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ أَثَرَكِ اللَّهُ عَلَيْنَا وَإِنْ كُنَّا لَخَطِيئِينَ ٩١

83. Mwenye kuharibu jina lake haaminiwi tena. Tujitahidi tusiharibu majina yetu idumu iibari yetu. Iibari ni kitu kikubwa kabisa.

92. Akasema (Yusufu): “Hakuna lawama juu yenu leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwenye rehema zaidi kuliko wanaorehemu (wote).”

93. “Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke mbele ya uso wa baba yangu: naye atafunuka macho aone. Na nijieni (nyote) pamoja na watu wenu wote.”

94. Na ulipoondoka msafara (katika Misri), baba yao (huku Shamu) alisema: “Nasikia harufu ya Yusufu; lau si kuwa mnaitakidi nimeharibika akili (mgenisadiki).” (Mwenyezi Mungu alimfanyia muujiza huo wa kusikia harufu ya ile kanzu ya Nabii Yusufu kabla haijafika).

95. Wakasema: “Wallah! Ungali katika upotofu (upotevu) wako wa zamani (wa kumpenda tu Yusufu).”

96. Basi alipokuja mtoaji wa khabari njema, akaiweka (kanzu ya Yusufu) mbele ya uso wake, mara aliona akasema: “Je! Sikukwambieni kuwa mimi najua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyaiua?”

97. Wakasema: “Ewe baba yetu. Tuombe msamaha kwa dhambi zetu, bila shaka sisi tulikuwa wenye khatia.”

98. Akasema: “Khalafu (baada ya kumuona Yusufu na kutaka msamaha kwake kwa mliyomfanya) nitakuombeeni msamaha kwa Mola wangu; hakika Yeye ndiye Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.” (Wakasafiri wote wakenda (Misri)).

99. Na walipoingia kwa Yusufu aliwakumbatia wazazi wake na akasema “Ingieni Misri, Inshaallah, mumo katika amani.”

100. (Na walipoingia kwa Yusufu), aliwainua wazazi wake na kuwaweka katika kiti (chake) cha ufalme. Na wote wakaporomoka kumsujudia. Na (Yusufu) akasema: “Ewe babaangu! Hii ndiyo (tafsiri) hakika ya ndoto yangu ya zamani. Bila shaka Mola wangu ameihakikisha. Na amenifanyia ihsani; akanitoa gereza na akakuleteni nyinyi kutoka jangwani; baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni Mwenye kulifikia alitakalo. Bila shaka Yeye ni Mjuzi na Mwenye hikima.”

92. Hivi ndiyo ndivyo—watu kusameheana hata yakiwa makosa gani, na yaliyopita yakapishwa, yasikumbushwe tena.

98. Ilivyokuwa hawakumfanyia ubaya sana yeye; lakini wamemfanyia zaidi Nabii Yusufu ndiyo amekawilisha kuwataka msamaha mpaka amuone Nabii Yusufu amuombe awasamehe nduguze.

100. Kusujudiana ndio maamkio makubwa ya kizamani. Sasa hapana ruhusa hata kurukiana. Na Kuna watu wanaosujudiwa wakabusiwa nyayo, nao kimya.

قَالَ لَا تَثْرِيبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ٩٢

إِذْ هَبُوا بَقِيصَ هَذَا فَالْقُوَّةُ عَلَى وَجْهِهِ
أَبَى يَأْتِ بِصِجْرَةٍ وَأَتَوْنِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ٩٣

وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيرُ قَالَ أَبُوهُمْ إِنِّي لَأَجِدُ
رَبِّيَ يُوسُفَ لَوْ كَا أَن تَقْدُودُن ٩٤

قَالُوا تَاللَّهِ إِنَّكَ لَفِي ضَلَالِكَ الْقَدِيمِ ٩٥

فَلَمَّا أَن جَاءَ الْبَشِيرُ أَلْفَهُ عَلَى وَجْهِهِ فَارْتَدَّ
بَصِيرًا قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَنَا عَالِمُ
مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ٩٦

قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ٩٧

قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ
الرَّحِيمُ ٩٨

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ أَوَّعَ إِلَيْهِ أَبَوَيْهِ وَقَالَ
ادْخُلُوا مِصْرًا إِن شَاءَ اللَّهُ أَمِينٌ ٩٩

وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا
وَقَالَ يَأْبَتِ هَذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِن قَبْلُ

قَبْلُ زَقَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا وَقَدْ أَحْسَنَ بِي إِذْ
أَخْرَجَنِي مِنَ السِّجْنِ وَجَاءَ بِكُم مِّنَ الْبَدْوِ مِن قَبْلِ

بَعْدِ أَنْ تَزْعُمَ الشَّيْطَانُ بَيْنِي وَبَيْنَ إِخْوَتِي إِنَّ
رَبِّي لَطِيفٌ لِّمَا يَشَاءُ إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ١٠٠

101. (Kisha akaomba dua akasema): “Ee Mola wangu! Hakika umenipa ufalme, na umenifundisha tafsiri ya maneno (ya ndoto na mengineyo). Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. (Wakati wa kufa) nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema.”

102. Hizi ni katika khabari za siri tulizokufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao, hali wakifanya vitimbi vibaya.

103. Na wengi katika watu hawatakuwa wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.

104. Wala huwaombi ujira juu ya haya; (na juu ya hivi hawataki kufuata). Hayakuwa haya (uliyokuja nayo) ila ni mauidha kwa walimwengu wote.

105. Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, na hali ya kuwa wanazipuza.

106. Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu isipokuwa na huku wanatia ushirikina.

107. Je! Wanaaminiisha kuwa hautawajia msiba wa adhabu ya Mwenyezi Mungu, au hakitawajia Kiama kwa ghafla, na hali hawatambui?

108. Sema: “Hii ndiyo njia yangu; ninaita (ninalingania) kwa Mwenyezi Mungu kwa ujuzi wa kweli; mimi (nafanya hivi) na (kila) wanaonifuata. Na Mwenyezi Mungu ametakasika na kila upungufu; wala mimi simo miongoni mwa wanaomshirikisha (Mwenyezi Mungu).”

106. Na haya hata petu hapa tunayo. Japo tunafuata Uislamu lakini tunatia ushirikina pia.

Tunakwenda makaburini takayaambia “Eee Bwana! Nimezongwa na . . . Ukinifungua . . . nitaleta hapa pesa au kombe la Haluwa au . . .” Anasikia wapi huyo maiti! Si bure tu wanabwabwatika! Mwenyezi Mungu amesema na kusema wee katika Qurani kuwa maiti hawasikii wambiwayo wala hawajui yapitayo duniani. Wao wana yao mbali kabisa.

Bali huwapigia kelele walio masafa baidi kabisa na wao, wakimwambia “Eee Bwana Fulani! Mtu wako mimi. Nitazame . . .” na kama hivi.

Kwani hao Mwenyezi Mungu, hata wamsikie anayewalingania popote pale akiwapo? Si itikadi ya Kiislamu hiyo. Anayesikia hivyo ni Mwenyezi Mungu tu.

108. Hapa anaambiwa Mtume awaambie viumbe kuwa yeye na kila wanaomfuata yeye hulingania watu maneno ya dini ya Uislamu kwa ujuzi wa kweli kweli, kwa hoja na dalili. Sio kusema kuwa “Mwendo wetu sisi Kuitakidi tu (ikiwa iko hoja na dalili na ujuzi au hapana).” Sio huu mwendo uliosema katika Qurani wala katika Hadithi za Mtume wala katika Maneno ya Wanavyuoni wote wa mbele huko.

Hana ruhusa Mwislamu kujifuatia tu pasi na hakika ya jambo hilo. Hana ruhusa kabisa Mwislamu kufanya hivi. Qurani dhahir shahir inasema. Usijifuatie tu jambo usilokuwa na ujuzi nalo maadamu hakulisema Mwenyezi Mungu au Mtumewe hata likiwa linafuatwa na Wazee na Maraisi. Si hoja hiyo kuwa linafuatwa na Wazee na Maraisi. Qurani yote nzima inasema kuwa si hoja hiyo kufuatwa na Wazee na Maraisi. Dini hiyo ya kufuata Wazee na Maraisi sio dini iliyoletwa na Uislamu.

رَبِّ قَدْ أَتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ، فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، أَنْتَ وَلِيَّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ ①

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ، وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَجْمَعُوا أَمْرَهُمْ وَهُمْ يَمْكُرُونَ ②

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ③

وَمَا تَسْأَلُهُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ، إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ④

وَكَايِنَ مِنَ آيَةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُّونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ⑤

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ⑥

أَفَأَمِنُوا أَنْ تَأْتِيَهُمْ غَاشِيَةٌ مِنْ عَذَابِ اللَّهِ أَنْ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ⑦

قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ عَلَى بَصِيرَةٍ، أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي، وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا آتَا مِنَ الشَّرِكِينَ ⑧

قَالَ اللَّهُ تَتْلُو شِعْرَ النَّاسِ لَمْ يَلِمْ بِهِمْ شَيْءٌ وَلَئِنْ كُنْتُمْ إِلَّا وَحْدَكُم مِمَّنْ يَنْتَحِبُونَ

109. Na hatukutuma (hatukuleta Mitume) kabla yako isipokuwa wanaume tuliowafunulia (tuliowaletea Wahyi; tena) katika watu wa miji. Je! Hawakutembea (hao makafiri) katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale (wabaya) waliokuwa kabla yao? Na nyumba ya Akhera ni bora kwa wale wamchao Mwenyezi Mungu. Je! Hamfahamu?

110. Hata Mitume walipokata tamaa, (na makafiri) wakadhani ya kwamba wameambiwa maneno ya uwongo (na hao Mitume, kwa kuona mbona haiji hiyo adhabu, hapo ndipo) msaada wetu ulipowajia (hao Mitume). Basi wakaokolewa tuliowataka. Na haiepushwi adhabu Yetu kwa watu waovu.

111. Bila shaka katika hadithi zao hizi limo fundisho kwa wenye akili. Si maneno yaliyozuliwa, bali ni hakikisho la yale yaliyokuwa kabla yake (miongoni mwa vitabu vyengine vya Mwenyezi Mungu) na ni maelezo pia ya kila kitu (kinachohitajiwa katika dini), na ni uwongofu na rehema kwa watu wenye kuamini.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رَجُلًا نُزِجَ إِلَيْهِمْ
مِّنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ ۚ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ
فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا ۖ
أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٠٩﴾


حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَكَانُوا الْأَنْهَامَ قَدْ
كُذِّبُوا جَاءَهُمْ نَصْرُنَا ۖ فَنُفِخَ بِالسَّاعَةِ وَلَا
يُرَدُّ بَأْسُنَا عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١١٠﴾

لَقَدْ كَانَ فِي قَصصِهِمْ عِبْرَةٌ لِأُولِي الْأَلْبَابِ ۚ
مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ وَلَكِنْ تَصْدِيقُ الَّذِي
بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَ
رَحْمَةً لِّلْقَوْمِ الْيُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾

﴿١١١﴾

110. Nusura ya Mwenyezi Mungu haiji unapoitaka tu, mpaka ufike wakati wake, sharti baada ya kumeza machungu kwanza walau kidogo. Basi usikate tamaa ikikawia nusura; itakuja tu. Baada ya Dhiki—hapana ila—Faraji.

111. Katika Aya hii waliyoifanya ya 112 wametia ukafiri wao wa kumdaia Utume na Unabii Isa huyo mtu wao. Tumeuvunja ukafiri huu katika Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na ya 4 za *Suratul Baqarah*. Na wakatia vile vile ukafiri wao wa kumdaia mtu wao huyo kumuona Mungu na kusema naye, kama walivyojaza katika chungu ya vitabu vyao.



Ina Aya 43

SURATUR RAAD

Ina Makuru 6

(Imeteremka Madina)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Mym Ra. Hizi ni Aya za hiki kitabu (kilichokusanya kila kinachohitajiwa). Na yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ndiyo haki, lakini watu wengi hawaamini.

الَّذِينَ نَزَّلَ إِلَيْكَ الْكِتَابَ وَالَّذِي أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ①

2. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziinua mbingu bila ya nguzo: mnazona hivi. Kisha akatawala juu ya Arshi (yake). Na akalitiisha (kwenu) jua na mwezi (akavifanya vitii). Kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliowekwa. Yeye ndiye anayeliendesha (kila) jambo. Anazipambanua Aya hivi ili mupate yakini ya kukutana na Mola wenu.

اللَّهُ الَّذِي رَفَعَ السَّيِّئَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ وَسَحَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ بَلَاغًا رَبِّكُمْ تُؤْتُونَ ②

3. Na ndiye aliyetitandaza ardhi na akaweka humo majabali na mito. Na katika kila matunda akafanya humo namna mbili (dume na jike). Huufunika usiku juu ya mchana (na mchana juu ya usiku). Hakika katika haya zimo Ishara (kubwa kuwa Mwenyezi Mungu yuko); kwa watu wenye kufikiri.

وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنْهَارًا وَمِنْ كُلِّ الشَّجَرِ جَعَلَ فِيهَا زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ يُغْثِي الْبَلَّ النَّهَارَ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ③

4. Na katika ardhi muna vipande vinavyoingana (na kuzaa kwake namna mbali mbali), na muna mabustani ya mizabibu, na mimea mingine, na mitende ichipuayo katika shina moja na isiyochipua katika shina moja. Vyote vinanoshelezwa (vinamiminiwa) maji yale yale; na tunavifanya bora baadhi yake vyengine katika kula (katika utamu). Hakika katika haya zimo ishara kwa watu wanaotia mambo akilini.

وَفِي الْأَرْضِ قَطْعٌ مُّتَبَعًا وَجَنَّاتٌ مِنْ أَعْنَابٍ وَزُرُوعٌ وَخَيْلٌ صِنْوَانٌ وَغَيْرُ صِنْوَانٍ يُسْقَى بِمَاءٍ وَاحِدٍ وَنُقْضِلُ بَعْضُهَا عَلَى بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ④

5. Na kama ukistaajabu, basi cha ajabu zaidi ni usemi wao: "Je! Tutakapokwisha kuwa udongo, kweli tutakuwa katika umbo jipya? (Hawezi Mungu

وَإِنْ تَعْجَبْ فَعَجَبٌ قَوْلُهُمْ إِذَا كُنَّا تُرَابًا مَا كُنَّا لِنُفْخَ بِخَلْقِ جَدِيدِهِ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا

3. Huyu Seyyidna Ahmad waliyemtaja katika maelezo yao ndiyo huyo mtu wao, na hiyo Safina ya Nuhu ni kimoja katika hivyo vitabu vyake vya kudaia na kujigamba madai yake. Kujigamba kiwatu Fulana. Na huyo jina lake Ghulam Ahmad, si Ahmad. Lakini sasa wanaliuwa tamko la Ghulam ili awe huyo Ismuhuu Ahmad.

5. Kuumbwa kwa tone la manii hawastaajabu! Wanastaajabu kuumbwa kwa mara ya pili kwa akitakacho Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Mtu mzima kufanyika kwa kidudu cha manii hawastaajabu.

kufanya hivi).” Hao ndio waliomkufuru Mola wao, na hao ndio yatakaokuwa makongwa katika shingo zao, na hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.

6. Na wanakuhimiza ulete mabaya (adhabu juu yao) kabla ya mema, hali ya kuwa zimekwishapita adhabu za namna zote kabla yao. Na hakika Mola wako ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya dhulma yao (dhambi zao), na hakika Mola wako (vile vile) ni Mkali wa kuadhibu.

7. Na husema wale waliokufuru: “Mbona hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola wake?” Hakika wewe ni Muonyaji; na kila kaumu ina muongozi (wake na namna yake ya kuongoza. Namna ya kuongoza kwako wewe ni kwa kuonyesha hoja na dalili si kuleta miujiza).

8. Mwenyezi Mungu anajua abebacho kila mwanamke (katika mimba yake) na yanavyoviza matumbo na yanavyozidisha (pia anajua). Na kila kitu kwake kwa kipimo (chake).

9. (Yeye ndiye) Mjuzi wa siri na dhahiri (na ndiye) Mkuu (na ndiye) aliye juu.

10. Ni sawa (kwake Mwenyezi Mungu), anayeficha kauli yake miongoni mwenu na anayeidhihirisha; na (pia) ajifichaye usiku na aendaye mchana. (Wote anawajua).

11. Ana (kila mtu) kundi (la Malaika) mbele yake na nyuma yake: wanamlinda (na kuyadhibiti anayoyafanya) kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anapowatakiwa watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yoyote badala yake (Mwenyezi Mungu).

12. Yeye ndiye anayekuonyesheni umeme kwa (kukutieni) khofu (ya kuuawa na radi) na tamaa (ya kupata mvua); na huyaleta mawingu mazito (ya kuleta mvua).

6. Katika ajabu ya makafiri hao ni kuwa wakiomba adhabu iwajie badala ya kuomba kheri. Wakisema—kama ilivyo katika Aya ya 32 ya *Suratul Anfal*—“Kama haya (aliyokuja nayo Muhammad) ni haki iokayo kwako, basi tupige kwa mvua ya mawe yanayotoka mbinguni au tulettee adhabu nyingine iumizayo (yoyote ile; lakini sisi hatufuati).” Na wakisema—kama ilivyo katika Aya ya 16 ya *Surat Sad*—“Mola wetu! Tulettee sehemu yetu ya adhabu kabla ya siku ya hisabu.” Na kama hivi kama ilivyotajwa katika Sura nyingine.

7. Waongo. Wanajidai kutaka miujiza hii na hii, wala hawafuati chochote.

11. Ukiona watu wanaharibikiwa sana na mambo yao basi ni kwa kuwa wao wenyewe wamebadilisha ule uliokuwa mwendo wao ukawapa hayo waliyokuwa nayo. Na lililo zaidi katika hayo ni Akhlaki (Mwendo, Tabia Sifa) zao.

Watu wanakuwa watu kwa Akhlaki zao. Wakiziharibu Akhlaki zao nzuri, kila chao kinaharibika. Anasema mshairi mmoja mkubwa kabisa “Watu huhisabika kuwa watu kwa zile Akhlaki zao nzuri. Wakiziacha akhlaki zao hizo basi na hayo huwaacha.”

يَرْبِّهِمْ ۚ وَأُولَٰئِكَ الْأَغْلَالُ فِيْ أَعْنَاقِهِمْ ۚ وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيْهَا خَالِدُونَ ﴿٥﴾

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ وَقَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمُ الْمَثَلُ ۚ وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُوْ مَقْعَدٍ لِلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ ۚ وَإِنَّ رَبَّكَ

لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٦﴾

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَّبِّهِ ۖ مَا تَأْتِيَنَّكَ مِنْدَرٌ وَكُلُّ قَوْمٍ هَادٍ ﴿٧﴾

اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنْثَىٰ وَمَا تَغِيصُ الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ ۚ وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِقَدَرٍ ﴿٨﴾

عِلْمُ الْغَيْبِ وَ الشَّهَادَةُ الْكَبِيرُ الْمُتَعَالِ ﴿٩﴾

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٠﴾

لَهُ مَعْقِدَاتٌ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ ۚ وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءَ آفَآ فَلَا مَرَدَّ لَهُ ۚ وَمَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ ءَالٍ ﴿١١﴾

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمْ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنْشِئُ السَّحَابَ الثِّقَالَ ﴿١٢﴾

13. Na radi inamsabihi Mwenyezi Mungu kwa kumshukuru na (pia) Malaika (husabihi) kwa kumuogopa. Na (Mwenyezi Mungu) hupeleka mapigo ya radi na kumpiga nayo amtakaye. Na hao (makafiri) wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu (kuwa yuko kweli au hayuko), na hali (ya kuwa yuko na) yeye ni Mkali wa kuadhibu.

14. Kwake ndiyo yako (maitikio ya) maombi ya haki. Na wale wanaowaomba badala yake (Mwenyezi Mungu kama mapango, mizimu na makaburi) hawawajibu chochote; bali (hali yao) ni kama yule anayenyosha mikono yake miwili kwenye maji ili yafike kinywani mwake; lakini hayafikii. Na hayako maombi ya makafiri ila katika upotofu

15. Na humsujudia Mwenyezi Mungu waliomo mbinguni na ardhi kwa khiari au kwa nguvu. Na (pia) vivuli vyao (vinamsujudia) asubuhi na jioni.

16. Sema: "Ni nani Mola wa mbingu na ardhi?" Sema: "Ni Mwenyezi Mungu." Sema: "Je, mnafanya waola wengine badala yake, ambao hawamiliki kwa ajili ya nafsi zao (kujivutia) nafuu wala (kujiondolea) dhara; (seuze kukufanyieni nyinyi?)" Sema: "Je, wanaweza kuwa sawa (wawili hawa) — kipofu na aonaye? Au vinaweza kuwa sawa (viwili hivi) — giza na nuru? Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika ambao wameumba kama alivyoumba Mungu; kwa hivyo viumbe (vya pande mbili hizo) vimewadanganikia?" Sema: "Mwenyezi Mungu ndiye Muumbaji wa kila kitu na ni mmoja tu, anayepitisha anayoyataka."

17. Ameteremsha maji kutoka mawinguni. Na mabonde yakapitisha maji kwa kadiri yake. Na mafuriko ya maji yakayachukua mapovu yaliyo juu ya maji. Na katika vile wanavyoyayusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo (kama dhahabu au fedha, huja) povu vile vile. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyotoa mfano wa haki na batili. Basi lile

وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ وَالْمَلَائِكَةُ مِنْ خِيفَتِهِ
وَيُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ يَشَاءُ
وَهُمْ يُجَادِلُونَ فِي اللَّهِ ۚ وَهُوَ شَدِيدُ الْحِسَابِ ۝

لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ ۚ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ
لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُمْ بِشَيْءٍ إِلَّا كَبَاسِطٌ كَفَيْهِ إِلَى
السَّمَاءِ لِيَبْتَلِيَ قَاهُ وَمَا هُوَ بِالْعَاجِزِ وَمَا
دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ۝

وَاللَّهُ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا
وَكَرْهًا وَظَلَمَهُمُ بِالْغُدُوِّ وَالْأَصَالِ ۝

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ قُلْ اللَّهُ قُلْ
أَنَا تَحَدُّثُكُمْ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءُ لَا يَتَذَكَّرُونَ
لَا أَنْفُسَهُمْ نَفْعًا وَلَا ضَرًّا قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَى
وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ وَالنُّورُ
أَمْ جَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ خَلَقُوا كَخَلْقِهِ فَتَشَابَهَ
الْخَلْقُ عَلَيْهِمْ قُلْ اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ
الْوَحِيدُ الْقَهَّارُ ۝

أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَالَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا
فَاتَّخَذَ السَّيْلُ رِبْدًا زَابِيًا وَمِمَّا يُوقَدُونَ
عَلَيْهِ فِي النَّارِ أَبْغَاءٌ حُلِيَّةٌ أَوْ مُتَنَاءٌ
زَبْدٌ مِثْلُهُ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْحَقَّ وَالْبَاطِلَ ۝

15. Hakuna yoyote asiyepitishiwa QAHARI ya Mwenyezi Mungu. Akamfanyia asilotaka. Kama hazitii amri za Mwenyezi Mungu za IBADA anazitii amri za Mwenyezi Mungu za RADA, kama kuugua, kuharibikiwa.

16. Hao wanaowaomba wowote wale—hata hao Masharifu walio makubani na Mashekhe—hawawezi kuwanufaisha wala kuwaondolea madhara.

17. Mara nyingi yasiyokuwa na nafuu ndiyo yanayokuwa na mshindo mkubwa, kisha yakadidimia; udhia ukesha; baada ya kuchukua muda katika kutaabisha.

povu linapita kama takataka tu basi; lakini vile vinavyowafaa watu vinakaa katika ardhi. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga mfano. (Kuwa hwenda ubaya ukapata nguvu lakini mwisho wake hupotelea mbali).

18. Watapata wema wale waliomuitika Mola wao. Na wale wasiomuitikia, hata kama wanalikuwa na vyote vilivyomo ardhini na (vingine) kama hivyo pamoja navyo, bila shaka wanalivitoa kujikombolea (wala hakitakubalika kikomboleo chao hicho). Hao watakuwa na hisabu mbaya, na makao yao ni Jahanamu. Na ni mahali pabaya palioje!

19. Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ni haki (akayafuata, basi) ni kama aliye kipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia.

20. (Nao ni hawa) Ambao wao hutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji ahadi (za wanaadamu wenzao)

21. Na ambao huyaunga aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe, na humuogopa Mola wao, na huiogopa hisabu mbaya (itakayowapata wabaya huko Akhera, kwa hivyo wakajitahidi kujiepusha na vitendo vyao hao wabaya).

22. Na ambao husubiri (wakastahmilia wenziwao) kwa kutaka radhi ya Mola wao, na wakasimamisha Sala na wakatoa katika vile tulivyowapa, (wakavitoa) kwa siri na dhahiri, na wakayaondoa maovu kwa mema. Hao ndio watakaopata malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera)

23. Mabustani ya milele watayaingia wao (pamoja) na waliofanya wema miongoni mwa wazee wao na wake wao na kizazi chao. Na Malaika wanawaingilia katika kila milango.

فَأَمَّا الرُّبُودُ فَيُضْرَبُونَ بِجُفَاءٍ، وَأَمَّا مَا يَنْفَعُ النَّاسَ فَيَكُفُّونَ فِي الْأَرْضِ، كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ ۝

لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ الْحُسْنَىٰ وَالَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُ لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّثْلَ مَعَهُ لَا قَتَدُوا بِهِمْ، أُولَٰئِكَ لَهُمْ سُوءُ الْحِسَابِ ۝ وَمَا أُولَٰئِكَ بِهِمْ جَهَنَّمَ، وَبِئْسَ الْيَهَادُونَ ۝

أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنَ رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ، إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولَٰئِكَ الْكِتَابِ ۝

الَّذِينَ يُؤْفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ، وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ ۝

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ۝

وَالَّذِينَ صَبَرُوا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً، وَيَدْرُؤُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ أُولَٰئِكَ لَهُمْ عُقْبَى الدَّارِ ۝

جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ۝

19-24. Zinatajwa sifa za watu wazuri na watakapoyapata. Basi natwende mwendo wao tuwe kama wao, tutengenekeke duniani na Akhera.

22. Kwa kusema 'Wakavitoa kwa siri na kwa dhahiri' kuonyesha kuwa hizo sadaka zake anazozitoa mtu asizitafutie wakati makhsusi, bali azitoe kwa kila namna. Zikihitaji kutolewa kwa siri — ili wasivunjike moyo hao wanaopewa — naatoe kwa siri. Na zikihitaji kutolewa kwa dhahiri — ili watu wengine wafuate kitendo hicho, kama katika michango ya dhahiri — basi naatoe kwa dhahiri.

Na kwa kusema 'Wakayaondoa maovu kwa mema' ni kubainisha kuwa watu hao wakifanyiwa mabaya, wao hawawalipi mabaya hao wanaowafanyia mabaya hayo, bali huendelea kuwafanyia yale yale mema waliyokuwa wakiyafanya.

Makadiyani katika Maelezo ya Aya waliyofanya kuwa ni ya 23 wametia uharibifu wa kusema kuwa inafaa kusali kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu — Qurani tu ndiyo isomwe kwa Kiarabu. Tahadharini na Mapotezo haya. Hakuna madhehebu iliyosema meneno haya waliyoyasema wao. Madhehebu zote zilizokuwa ni za Kiislamu kweli — zinasema kuwa (a) Qurani lazima isomwe kwa lugha ya Kiarabu na (b) kila kilichomo — na kinacholetwa — ndani ya Sala kisomwe kwa Kiarabu. Basi natutahadhari na kuharibiwa Sala zetu; Na Uislamu — baada ya

24. (Wanawaambia): "Salamun Alaykum"
 "Iwe amani juu yenu, kwa sababu mlisubiri
 (mlistahmili katika kufanya mema na kuacha mabaya
 na mkastahmilia mkakaa vizuri na wenzenu)." Basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba (ya Akhera kwa wanaomcha Mungu).

25. Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu (na za wanaadamu wenzao) baada ya kuzifunga, na wanakata aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanafanya uharibifu katika nchi; hao ndio watakaopata laana, na watapata nyumba mbaya.

26. Mwenyezi Mungu hukunjua riziki kwa amtakaye na huidhikisha (kwa amtakaye). Na wamefurahia maisha ya dunia (ya mambo mabaya kuliko ya Akhera). Na uhai wa dunia kwa mkabala wa Akhera si kitu ila ni starehe ndogo tu.

27. Na wanasema wale waliokufuru: "Kwa nini hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola wake?" Sema: "Hakika Mwenyezi Mungu humuachia apotee amtakaye (kwa kuwa hataki kuelekea kwake) na huwongoza wanaoelekea kwake.

28. (Nao) ni wale walioamini na zikatulia nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia.

29. Wale walioamini na kufanya vitendo vizuri raha itakuwa yao, na marejeo mema."

30. Namna hivi tumekuleta katika watu ambao wamekwishapita kabla yao watu wengine (na wamesikia habari zao), ili uwasomee tunayokufunulia. Na wao wanamkufuru (Mwenyezi Mungu) Rahmani. Sema: "Yeye ndiye Mola wangu, hakuna aabudiwaye (kwa haki) ila Yeye; nimemtegemea yeye; na marejeo yangu ni kwake. (Na nyinyi fanyeni vivi hivi kwani huyo ndiye Mola wenu pia)."

31. Na kama ingalikuwako Qurani ambayo kwa Qurani hiyo milima ingaliondoshwa (inaposomwa),

سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرُ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوْصَلَ وَ يَفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ أُولَٰئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٥﴾

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَ يَقْدِرُ وَ فَرَحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَ مَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَاعٌ ﴿٢٦﴾

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ قُلْ إِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ أَرَادَ ﴿٢٧﴾

الَّذِينَ آمَنُوا وَ تَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾

الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَى لَهُمْ وَحَسُنَ مَا أَتَى ﴿٢٩﴾

كَذَٰلِكَ أَرْسَلْنَا فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهَا أُمَمٌ لِنَتْلُوَ عَلَيْهِمُ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ قُلْ هُوَ رَبِّي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ مَتَابٌ ﴿٣٠﴾

وَلَوْ أَنَّ قُرْآنًا سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ أَوْ قُطِعَتْ بِهِ

Shahada — ni Sala. Wameiharibu Shahadatu Anna Muhammadar Rasuulul Lah; sasa wanaingia kuiharibu na Sala — Udhia wishe.

25. Wanatajwa walio kinyume na wale na yatakayowafika. Tusiwe kama wao.

26. Kwa kuwatazamia maslaha yao—huyu maslaha kwake ni ufakiri, huyu maslaha kwake ni utajiri.

31. Lakini siyo kazi ya Qurani. Kazi ya Qurani ni kuongoza mwendo wa kutengeneza Akhera na Dunia.

au kwa hiyo ardhi ingalipasuliwa, au wafu wangelisemeshwa kwa hiyo (basi ingekuwa Qurani hii ndiyo ya kufanya kazi hiyo, lakini hiyo siyo kazi ya Qurani). Siyo! Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Je! Hawajajua walioamini ya kwamba Mwenyezi Mungu angalipenda bila shaka angaliwaongoza (Uislamuni) watu wote? (Akawaumba kama Malaika, hawana matamania. Lakini amewapa akili na matamania wapigane baina ya viwili hivi, washinde waingie Peponi). Wala msiba hautaacha kuwapata wale waliokufuru kwa sababu ya yale waliyoyafanya, au utashuka karibu na nchi zao, mpaka ifike ahadi ya Mwenyezi Mungu (ya kuwatoa roho). Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi (yake).

32. Na kwa yakini walichezwa shere (walifanyiwa mizaha vile vile) Mitume waliokuwa kabla yako. Na nikawapururia (sikuwatesa upesi) wale waliokufuru, kisha nikawatia mkononi. Basi ilikuwaje adhabu (yangu)!

33. Je! Anayeisimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma (ili ailipe, siye wa kuabudiwa)? Wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika. Sema: "Watajeni (washirika hao). Au je, mnamwambia asiyoajua katika ardhi; au ni maneno matupu (tu hayo mnayoyasema, yamo midomoni mwenu tu, hayamo katika itikadi yenu)?" Bali wamepambiwa makafiri uzushi wao huo, na wakazuiliwa njia (ya haki). Na ambaye Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea hana muongozi (mwengine wa kumuongoa).

34. Wanayo adhabu katika maisha ya dunia; na bila shaka adhabu ya Akhera ni ngumu zaidi wala hawatakuwa na mlinzi kwa Mwenyezi Mungu.

35. Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wamchao Mwenyezi Mungu (ni hivi): mbele yake inapita mito, matunda yake ni ya daima na (pia) kivuli chake. Huu ndio mwisho wa wale wamchao Mungu. Na mwisho wa makafiri ni Moto.

36. Na (baadhi ya) ambao tuliwapa Kitabu (Nao ni Mayahudi na Manasara) wanafurahia

الْأَرْضُ أَوْ كُلِّمَ بِهِ الْمَوْتِ بَلْ لِلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا
أَفَلَمْ يَأْتِ الْبَشَرِ الْأَمْنُ أَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ
لَهَدَى النَّاسَ جَمِيعًا وَلَا يَزَالُ
الَّذِينَ كَفَرُوا يُصِيبُهُمْ بِمَا صَنَعُوا قَارِعَةٌ أَوْ تَحُلُ
قَرْنًا مِّنْ دَارِهِمْ حَتَّىٰ يَأْتِيَ وَعْدُ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ لَا
يُخْلِفُ الْوَعْدَ ۝

وَلَقَدْ اسْتَهْزَيْ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَمَلَيْتُ
لِلَّذِينَ كَفَرُوا ثُمَّ أَخَذْتَهُمْ فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ۝

أَفَمَن هُوَ قَائِمٌ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ
وَجَعَلَ اللَّهُ شُرَكَاءَ ۝ قُلْ سَوَّهْمُ أَمْرٌ تُكَيِّدُ
بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي الْأَرْضِ أَمْ يَبْطِئُ هَاهُنَا مِنَ الْقَوْلِ
بَلْ رُبَّمَا لَئِيْن كَفَرُوا مَكَرُهُمْ وَصَدَّوْا
عَنِ السَّبِيلِ ۝ وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ۝

لَهُمْ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَقُّ
وَمَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مِن وَّاقٍ ۝

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ۝ تَجْرِي مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۝ أُكْلُهَا دَائِمٌ وَظِلُّهَا ۝ تِلْكَ عُقْبَى
الَّذِينَ اتَّقَوْا ۝ وَعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ ۝

وَالَّذِينَ آمَنُوا أَلَيْسَ لَهُمْ الْكِتَابُ بِفَرَحٍ ۝ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ

Na tumebainisha katika Aya ya 125 ya *Suratul An-Am* wanaoongolewa na Mwenyezi Mungu na wasioongolewa.

Hizo tafsiri za "Aali Jibal" na ya hayo matamko mengine waliyoyataja Makadiyani katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 32, siyo kabisa tafsiri iliyokusudiwa hapa. Wanataka kupoteza tu na kujaza farumu, ionekane kubwa hiyo tafsiri yao (taghiviri yao).

uliyoteremshiwa (na wamesilimu na wanayafuata). Na katika makundi yao (makafiri) mengine wako wanayoyakataa baadhi ya haya. Sema: "Nimeamrisha kumuabudu Mwenyezi Mungu tu wala nisimshirikishe. Ninaita Kwake (Mwenyezi Mungu viumbe wenzangu waongoke kama nilivyoongoka). Na ni Kwake marejeo yangu."

37. Na namna hivi tumeiteremsha (hii Qurani), hali ya kuwa ni hukumu (ya Mungu iliyoteremka) kwa (lugha ya) Kiarabu. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya kukufikia ilimu hii, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.

38. Na tuliwapeleka Mitume kabla yako, na tukawajaalia kuwa na wake na watoto; (si kiroja ukiwa Mtume wewe una wake na watoto). Na haiyumkiniki kwa Mtume kuleta miujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unayo hukumu aliyoiandika Mwenyezi Mungu, (ukitimu muda huo itafika hukumu hiyo).

39. Mwenyezi Mungu hufuta ayatakayo na huthubutisha (ayatakayo). Na asili ya hukumu zote iko kwake (Mwenyezi Mungu).

40. Na kama tukikuonyesha baadhi ya (adhabu) tuliyowaahidi (kuwatia hao wabaya) au tukikufisha (kabla hujaijua, wao itawafika tu). Basi juu yako ni kufikisha tu (uliyomamrisha kuyafikisha), na juu yetu ni kuwahisabu (siku ya Kiama).

41. Je! Hawakuona kwamba tunaifikia ardhi yao (makafiri), tunaipunguzapunguza katika mipaka yake? Na Mwenyezi Mungu huhukumu (kwa uadilifu) na hakuna wa kupinga hukumu Yake. Naye ni mwepesi wa kuhisabu.

42. Na walifanya hila wale (makafiri) waliokuwa kabla yao (makafiri hawa); lakini (kupindua) hila zote ni kwa Mwenyezi Mungu. Anajua anayoyachuma kila kiumbe. Na makafiri watajua matokeo (mema) ya nyumba (ya Akhera) yatakuwa ya nani!

43. Na wanasema waliokufuru: "Wewe si Mtume." Sema: "Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na baina yenu (kuwa mimi ni Mtume) na (pia) yule mwenye ilimu ya Kitabu. (Kila aliyeisoma Taurati iliyo sahihi na Injili iliyo sahihi ameziona khabari za Nabii Muhammad humo)."

وَمِنَ الْأَحْزَابِ مَنْ يُتَكَرَّرُ بَعْضُهُ قُلْ إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ وَلَا أُشْرِكَ بِهِ إِلَيْهِ أَدْعُوا وَإِلَيْهِ مَآبٌ ۝

وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ حُكْمًا وَعَذَابًا ۚ وَلَئِنْ أَتَيْتَ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ۚ لَا يَقِي ۝

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً ۚ وَمَا كَانَ لِرُسُلِ أَنْ يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ ۝

يَسْأَلُونَ اللَّهَ مَا يُشَاءُ وَيُخْفَتُونَ ۚ وَعِنْدَهُ أُمُ الْكِتَابِ ۝

وَلَا تَمَّا يُرِيدُكَ بَعْضُ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ تَتَوَقَّيْتُكَ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاءُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ۝


أَلَمْ يَرَوْا أَنَّا تَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا ۚ وَاللَّهُ يَحْكُمُ لَا مُعَقِّبَ لِحُكْمِهِ ۚ وَهُوَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ۝

وَقَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَلِلَّهِ الْمَكْرُ جَمِيعًا يَعْلَمُ مَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ وَسِعَ الْعِلْمُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۚ عَلِيمٌ غَفُورٌ ۝

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَسْتَ مُرْسَلًا ۚ قُلْ كَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۚ وَمَنْ عِنْدَهُ عِلْمُ الْكِتَابِ ۝

۝

38. Ati wanastaajabu kumuona Mtume ana wake na watoto. Mitume wote walikuwa na wake na watoto ila Nabii Yahya na Nabii Isa.



Ina Aya 52

SURAT IBRAHIM

Ina Makara 7

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Alif Lam Ra. (Hiki ni) Kitabu tulichokiteremsha kwako ili uwatowe watu katika giza uwapeleke katika nuru, kwa idhini ya Mola wao, uwafikishe katika njia ya yule Mwenye kushinda Mwenye kusifiwa (Naye ni Mwenyezi Mungu)

2. Mwenyezi Mungu, ambaye ni vyake peke yake vyote vilivyomo katika mbingu na katika ardhi. Na mateso yatawathubutikia makafiri kwa adhabu iliyo kali (inayowangoja)

3. Wale wanaofadhilisha maisha ya dunia kuliko Akhera, na wakawazuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotoa (na hali ya kuwa si potofu). Hao wamo katika upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).

4. Na hatukumpeleka Mtume yoyote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia. Kisha Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea amtakaye (kwa kuwa mwenyewe hataki kuongoka), na humuongoza amtakaye. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

5. Na tulimpeleka Musa pamoja na miujiza yetu: (tukamwambia): "Watoe watu wako katika giza kuwapeleka katika nuru, na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu. Bila shaka katika hayo muna mazingatio kwa kila anayevumilia na kushukuru."

6. Na (wakumbushe watu wako) aliposema Musa kwa watu wake: "Kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu; alipokuokoeni kwa watu wa Firauni, waliokupeni adhabu mbaya, na wakawachinja watoto wenu wanaume na wakawaacha hai watoto wenu wanawake. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa unaotoka kwa Mola wenu."

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّحْمَنُ كَتَبَ الرُّسُلَ إِلَيْكَ لِيُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَى صِرَاطٍ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ١

اللَّهُ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمُوتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۚ وَوَيْلٌ لِلْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ٢

الَّذِينَ يَسْتَحِبُّونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا أُولَئِكَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ٣

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رُسُولٍ إِلَّا بِلِسَانٍ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضِلَّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ٤

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَى بِآيَاتِنَا أَنْ أَخْرِجْ قَوْمَكَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَذَرِكْهُمْ بِالْآيَاتِ ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ٥

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ أَنْجَاكُمْ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ وَيَدْعُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ وَفِي ذَلِكَ لَكُمْ بَلَاءٌ مِنْ رَبِّكُمْ عَظِيمٌ ٦

3. Hakatazwi mtu kuishughulikia dunia yake; lakini Akhera ndio mbele.

4. Tumebainisha katika Aya ya 125 ya Suratul An-Am wapi Mwenyezi Mungu anawaongoza na wapi anawaachia kupotea.

7. Na (kumbukeni) alipotangaza Mola wenu (kuwa) "Kama mkishukuru, nitakuzidishieni; na kama mkikufuru, (jueni) kuwa adhabu Yangu ni kali sana."

8. Na Musa alisema: (Kuwaambia watu wake): "Kama mtakufuru nyinyi na waliomo katika ardhi wote, (hajali kitu Mwenyezi Mungu). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na ni Mwenye kustahiki."

9. Je! Hazikukujieni habari za wale waliokuwa kabla yenu? Watu wa Nuhu na Adi na Thamudu na wale wa baada yao ambao hakuna awajuaye ila Mwenyezi Mungu? Waliwajia Mitume wao kwa hoja zilizo waziwazi. Wakarudisha mikono yao juu ya vinywa vyao, na wakasema (kuwaambia Mitume hao) "Hakika sisi tunayakataa mliyotumwa nayo. Na hakika sisi tunayo shaka ituhangaishayo kwa hayo mnayotuitia (ya kumuabudu Mwenyezi Mungu mmoja)."

10. Mitume wao wakasema: "Je! Mnamfanyia shaka Mwenyezi Mungu. Muumba wa mbingu na ardhi? Yeye anakuiteni akusamheheni dhambi zenu na akupeni muhula mpaka muda uliowekwa." Wakasema: "Hamkuwa nyinyi ila ni watu kama sisi. Mnataka tu kutuzuilia na yale waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu. Basi tuletteeni hoja zilizo wazi."

11. Mitume wao wakawaambia: "Sisi hatukuwa ila ni watu kama nyinyi (kama mnavyosema). Lakini Mwenyezi Mungu huwafanyia ihsani awatakao katika waja wake (akawapa Utume). Wala sisi hatuwezi kukuleteeni hoja hizo (mnazozitaka) isipokuwa kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu. Na kwa Mwenyezi Mungu wategemee Waislamu (wote)."

12. "Na tuna nini tusimategemee Mwenyezi Mungu, na hali ametuonyesha njia zetu. Na tutayavumilia mnayotuudhia. Basi kwa Mwenyezi Mungu tu wategemee wategemeao."

13. Na wale waliokufuru wakawaambia Mitume yao: "Tutakutoeni katika nchi yetu au lazima murudi katika mila yetu." Basi Mola wao akawaletea wahyi kuwa "Tutawaangamiza madhalimu"

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِنْ شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِنْ كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ①

وَقَالَ مُوسَى إِنَّ تُكْفَرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَإِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ ②

أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَثَمُودٌ وَالَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا اللَّهُ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَرَدُّوا أَعْيُنَهُمْ فِي أَقْوَامِهِمْ وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ وَإِنَّا لَفِي شَكٍّ مِمَّا تَدْعُونَنَا إِلَيْهِ مُرِيبٌ ③

قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِى اللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُمْ وَنَّ دُنُوبَكُمْ وَيُخَوِّدَكُمْ إِلَى أَجَلٍ مُّسَمًّى قَالُوا إِنَّا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا تُرِيدُونَ أَنْ تَصُدُّونا عَنْ مَا كَانُوا يَعْبُدُ آبَاءَنَا فَأَتُونَا بِسُلْطَانٍ مُبِينٍ ④
قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ إِنَّا نَعْنُ إِلَّا بِشَرٍّ مِثْلَكُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَمُنُّ عَلَى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَمَا كَانَ لَنَا أَنْ نَأْتِيَكُمْ بِسُلْطَانٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ⑤

وَمَا لَنَا أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى اللَّهِ وَقَدْ هَدَانَا سُبُلَنَا وَلَنَصْبِرَنَّ عَلَى مَا أَدَّيْتُمُونَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ⑥
وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِرُسُلِهِمْ لَنُخْرِجَنَّكُمْ مِنْ أَرْضِنَا أَوْ لَتَعُولَنَّ فِيهِمْ وَلَتَمُوتُنَّ قَاتِلًا أَلَيْسَ لِرَبِّهِمْ كُنُوزٌ الْعَالَمِينَ ⑦

7. Kuishukuru neema khasa na kuzitumia mahala pake sio kusema *Alhamdu Lillahi* tu: Na ubaya mkubwa kabisa kuzitumia kwa maasi.

10. Katika hii Aya waliyoifanya ya 11 wameifasiri *Faatir* wanavyotaka wao.

12. Mwislamu kila siku inataka amategemee Mwenyezi Mungu, baada ya kwisha kujiweka tayari kama alivyomuamrisha Mungu.

14. "Na tutakukalisheni (nyinyi) katika nchi (hizi) baada yao." Watapata haya wale waliogopa kusimamishwa mbele yangu na wakaogopa maonyo yangu (Kwa hivyo wakafanya mema na wakajiepusha na mabaya).

15. Na walitafutatafuta (kila njia za kuushinda Uislamu, wasizipate), na akashindwa kila jabari mkaidi

16. Ambaye mbele yake kuna (adhabu ya) Jahannamu na atanyweshwa (huko) maji ambayo ni usaha (na damu yao wenyewe humo Motoni)

17. Awe anayagugumiza wala hawezi kuyameza. Na (sababu za) mauti zitamjia kutoka kila mahali, naye hatakufa. Na zaidi ya hayo iko adhabu (nyengine) kali (vile vile).

18. Mfano wa wale waliomkufuru Mola wao: vitendo vyao (vyema ambavyo havilipwi kheri kwa kuwa hawakuwifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu) ni kama jivu linalopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya upepo mkali. Hawataweza kupata chochote katika waliyoyafanya. Huo ndio upotofu (upotevu) ulio mbali kabisa.

19. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki? Akitaka atakuondoeni (mara moja) na kuleta viumbe (wengine) wapya

20. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si gumu.

21. Na wote watahudhuria kwa Mungu (ili awalipe). Hapo wanyonge (waliopotea kwa ajili ya kuwafuata wakubwa wao) watasema kuwaambia wale (wakubwa wao) waliojivuna (wakaikataa haki): "Sisi tulikuwa tukikufuateni nyinyi; basi je, nyinyi mnaweza kutuondolea kitu kidogo hivi katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?" Watasema: "Angalituongoza Mwenyezi Mungu bila shaka tungalikuongozeni. (Lakini sasa) ni mamoya kwetu: tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia."

22. Na Shetani atasenia itakapokatwa hukumu (ya wema kwenda Peponi na wabaya kwenda Motoni; atawaambia wale maasi watakaomng'ang'ania): "Mwenyezi Mungu alikuahidini ahadi ya kweli (na leo ameitimiza), nami nilikuahidini; lakini sikukutimizieni. Wala sikuwa na

وَلَنُكَلِّمَنَّكُمْ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِهِمْ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَافَ مَقَامِي وَ خَافَ وَعِيدِ ۝

وَأَسْتَفْتُوا وَ خَابَ كُلُّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ ۝

مَنْ وَرَّاهُ جَهَنَّمَ وَ يُلْقَىٰ مِنْ مَّاءٍ صَدِيدٍ ۝

يَجْعَلُهُ وَلَا يَكَادُ يُسِغُهُ وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ وَمَا هُوَ بِمَيِّتٍ وَمِنْ وَرَائِهِ عَذَابٌ غَلِيظٌ ۝

مِثْلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ أَعْمَالُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ لَا يَقْدِرُونَ مِمَّا كَسَبُوا عَلَىٰ شَيْءٍ ذَٰلِكَ هُوَ الصَّلُّ الْبُعِيدُ ۝

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ إِنَّ يَٰسَأُ يُدْهِبُكُمْ وَ يَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ۝

وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ۝

وَبَرَّرُوا اللَّهَ جَمِيعًا فَقَالَ الضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنْنا مِنَ عَذَابِ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ قَالُوا كُوهْدَنَا اللَّهُ لَهْلَيْنَاكُمْ سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَجْرُنَا أَمْ صَبْرُنَا مَا لَنَا مِنْ مَحْصِنٍ ۝

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعْدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ

14. Anayeyachelea haya hujitengeneza barabara; akatengenekeza Akhera na duniani.

18. Anayeupinga Uislamu — na hali ya kuwa anajua kuwa ndiyo dini ya haki — hayakubaliwi mema yake anayoyafanya.

21. Yatakayotokea baina ya wafuasi na wafuatwa.

mamlaka juu yenu (ya kukulazimisheni kunifuata); isipokuwa nilikwiteni tu, nanyi mkanitika. Basi msinilaumu, bali jilaumuni wenyewe: siwezi kukusaidieni wala nyinyi hamuezi kunisaidia. Hakika mimi nilikataa kunishirikisha kwenu toka zamani.” Kwa yakini madhalimu watakuwa na adhabu iumizayo.

23. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri wataingizwa katika Mabustani yapitayo mito mbele yake, wakae milele humo kwa idhini ya Mola wao. Maamkiano yao humo yatakuwa (Salaamun Alaykum za kila upande, yaani Amani tu juu yenu na furaha na salama).

24. Je! Hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri (ambao) mizizi yake ni imara na matawi yake yamenyoka juu

25. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake; (basi ndivyo neno zuri linavyoleta kheri). Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka.

26. Na mfano wa neno baya ni kama mti mbaya ambao umeng'olewa katika ardhi, hauna imara.

27. Mwenyezi Mungu huwathubutisha wale walioamini kwa kauli thabiti, katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu (nafsi zao). Na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo (kwani kila alifanyalo ni ia kheri tu).

28. Je! Hukuwona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kukufuru; na wakawafikisha watu wao (waliowafuata katika mabaya yao) katika nyumba ya maangamizo

وَمَا كَانَ لِيَ عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطَانٍ إِلَّا أَنْ دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِيْهِ فَلَا تُلْمُونِيْ وَلَوْلَا أَنْفُسُكُمْ مَا آتَاكُمْ بِصُحُفِكُمْ وَمَا أَنْتُمْ بِعَصْرِيٍّ إِلَيَّ كَفَرْتُمْ بِمَا أَنْزَلْنَاكُمْ مِنْ قَبْلُ إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ٢٣

وَأَدْخِلِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ تَحِيَّةٌ لَهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ٢٤

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ٢٥

تُؤْتِي أَكْثَرَهَا ثَمَرًا كُلٌّ مِنْ إِذْنِ رَبِّهَا وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ٢٦

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ مِنْ قُوتٍ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ٢٧

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ٢٨

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ٢٩

24-25. Inapigiwa mfano kheri namna inavyotanda vizuri ikaleta nafuu kila upande.

25. Katika Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 26 wamepachika chungu ya maneno yasiyokuwa na haja; na mwisho wakatia waliolikusudia. Nalo ni kudai kuwa Utume unaendelea. Wakaandika hivi:— “Katika zama zote zilizopita imetoa watu ambao, kwa kuifuata, wakaweza kujiunganisha na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu akazungumza nao sana. Watu wa namna hii wataendelea kutokea katika wafuasi wa Qurani.” Huu ni ukafiri. Na tumeurejea katika Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na ya 4 ya *Suratul Baqarah*, na katika Aya ya 157 ya *Suratul Aaraf*.

26. Inapigiwa mfano shari namna inavyotanda juu tu — kama miti ya kutambaa — kisha ikasukulikia mbali, ikapotea.

27. Aliye kigeugeu hapa (mnaifiki) atababaika kote huko, aingie Motoni.

28. Katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 29 wamefanya kusudi kulifasiri uwongo tamko la *Nimatal Lah* ili wamdaie Utume mtu wao.

29. (Ambayo ni) Jahannamu. Wataingia; na ni mahali pabaya kabisa pa kukaa (kiumbe).

30. Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili kupoteza (watu) katika njia yake. Sema: "Jifurahisheni kidogo tu, kisha marejeo yenu ni katika Moto."

31. Waambieni waja wangu walioamini, wasimamishe Sala, na watoe katika vile tulivyowaruzuku, kwa siri na kwa dhahiri, kabla haijafika siku isiyokuwa na (msaada unaopatikana kwa) kujikomboa wala urafiki.

32. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi na akateremsha maji kutoka mawinguni. Na kwa hayo akaotesha matunda kuwa riziki kwa ajili yenu. Na akakutiishieni majahazi ili yapite katika bahari kwa amri yake, na akakutiishieni mito.

33. Na akakutiishieni jua na mwezi, maisha yao (yanafanya yaliyoamrisha, ya kuchomoza na kuchwa na mengineyo kwa ajili ya manufaa yenu). Na akakutiishieni usiku na mchana.

34. Na akakupeni kila mlichomuomba (na msichomuomba). Na kama mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamtaweza kuzihisabu. Bila shaka mwanaadamu ni dhalimu mkubwa asiye shukrani (mwizi wa fadhila).

35. Na (kumbukeni) aliposema Ibrahimu: "Mola wangu! Ujaalie mji huu (wa Makka) uwe wa amani. Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu."

36. "Mola wangu! Hakika (masanamu) hawa wamepoteza watu wengi. Basi aliyenifuata ni wangu mimi (utamlipa mema kama ulivyotuahidi); na aliyeniasi (unaweza kumsamehe pia usimtese) kwani Wewe ni Mwingi wa msamaha na Mwingi wa rehema."

37. "Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka (nimewakalisha baadhi kizazi changu (mwanangu Ismaili na mama yake, Hajara) katika bonde (hili la Makka) lisilokuwa na mimea yoyote; katika nyumba yako takatifu (ya Al Kaaba utakayotwambia tuijenge)

جَهَنَّمَ، يَصْلَوْنَهَا وَيُنْسِ الْقَرَارُ ①

وَجَعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّيُضِلُّوا عَنْ سَبِيلِهِ
قُلْ تَتَّبِعُوا فَإِنِّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ ②

قُلْ لِعِبَادِيَ الَّذِينَ آمَنُوا يُقِيمُوا الصَّلَاةَ
وَيُنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً مِّن قَبْلِ
أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خِلْ ③

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ مِنَ
السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ
وَسَخَّرَ لَكُمُ الْفُلْكَ لِتَجْرِيَ فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ
وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ④

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَلِيلَيْنِ، وَسَخَّرَ لَكُمُ
الْيَلَّ وَالنَّهَارَ ⑤

وَإِنكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ
لَا تَحْصُوهَا إِنَّ الْإِنسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ⑥

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ
أَمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعْبُدَ الْأَصْنَامَ ⑦

رَبِّ إِنِّي أَصْلَحْتُ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ، فَمَنْ
تَبِعَنِي فَإِنَّهُ مِنِّي، وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ
رَّحِيمٌ ⑧

رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بُيُوتًا غَيْرَ ذِي
زَمْرٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ

32-34. Anawatajia baadhi ya neema zake zilizo dhahiri na anawaachia wazikumbuke zisizotajwa.

37. Kauli yenye nguvu iliyothubutu kwa maneno ya Qurani na ya Hadithi sahihi za Mtume ni kuwa Al Kaaba imejengwa na Nabii Ibrahimu na Nabii Ismaili yapata miaka elfu sita sasa, siyo imejengwa na Nabii Adamu au Malaika. Kauli hiyo haikuthubutu kwa Qurani wala kwa Hadithi sahihi za Mtume.

Mola wetu! Wajaalie wasimamishe Sala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao (wapende kuja kukaa hapa ili pawe mji) na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru.”

38. “Mola wetu! Hakika wewe unajua tunayoyaficha na tunayoyadhihirisha. Na hakuna chochote kinachofichikana kwa Mwenyezi Mungu katika ardhi wala katika mbingu.”

39. “Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee (wangu watoto wawili hawa:-) Ismaili na Is-haqa. Hakika Mola wangu ni Mwenye kusikia maombi (ya waja wake. Naliomba kizazi akanipa).”

40. “Mola wangu! Nijaalie niwe msimamishaji Sala, na kizazi changu (pia kiwe hivi) Mola wetu! Na upokee maombi yangu (mengine).

41. “Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili na wanaoamini; siku ya kusimama hisabu (Kiama).”

42. Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilia na (haya) wanayoyafanya madhalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku ambayo macho (yao) yatakodoka (yatoke nje kwa khofu)

43. (Wawe) wanakwenda mbio, vichwa juu, na macho yao hayapepesi, na nyoyo zao tupu (haziko, wanahemkwa mbio, mapepe)!

44. Na uwaonye watu siku ambayo itawafikia adhabu, waseme waliodhulumu (nafsi zao) “Mola wetu! Tuakhirishe muda mdogo. Tutaitikia wito wako na tutawafuata Mitume.” (Waambie) “Je! Hamkuwa mumeapa zamani ya kwamba nyinyi hamtapata muhamo wowote (wa kuihama dunia)?”

فَجَعَلَ أَفْنَدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَارْتُفِعَتْ
مِنَ الشَّجَرَاتِ لَهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٨﴾

رَبَّنَا إِنَّكَ تَعْلَمُ مَا نُخْفِي وَمَا نُعْلِنُ وَمَا يَخْفَى
عَلَى اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿٣٩﴾

أَحْمَدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ
وَلِإِسْحَاقَ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٤٠﴾

رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي ۚ رَبَّنَا
وَقَبَّلْ دُعَاءِ ﴿٤١﴾

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ
يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٤٢﴾

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَافِلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۚ
إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمَ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ ﴿٤٣﴾

مُهْطِعِينَ مُقْنِعِي رُؤُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ
طَرْفُهُمْ ۚ وَانفِثْهُمْ هَوَاءً ﴿٤٤﴾

وَأَنذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ
فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا آخِرْنَا إِلَىٰ آجَلٍ
قَرِيبٍ يُجِيبُ دَعْوَتَكَ وَتَتَّبِعُ الرُّسُلَ ۗ أَوَلَمْ تَكُونُوا
أَقْسَمْتُمْ مِّنْ قَبْلِ مَا لَكُم مِّنْ زَوَالٍ ﴿٤٥﴾

40. Nguzo kubwa ya Uislamu kama tunavyojua—ni Sala.

41. Mwislamu wa kweli—kama anavyojishughulikia yeye mwenyewe na kuwashughulikia walio wake—inataka awashughulikia na Waislamu WOTE wenzake kwa kiasi cha uweza wake. Hapa Nabii Ibrahimu—kama alivyojiomba msamaha yeye na wazee wake—anawaomba msamaha Waislamu wote. Na ameyafanya haya Nabii Nuhu kama ilivyo katika mwisho wa Surat Nuhu. Basi natukamatane na dua zao hizi. Na watafanya haya pia siku ya Kiama Mitume hawa wawili na wengine kama ilivyo katika Qurani na Hadithi za Mtume sahihi.

42. Tunaona katika Qurani yote kuwa Mwenyezi Mungu hawatesi wabaya upesi. Anawapa muda mkubwa ili wapate fursa ya kurejea kwake kabla ya kuteremkiwa na adhabu. Mwenyezi Mungu Rahimu.

44. Lakini ukisha kufika muda wa kuadhibiwa, hapo hawapewi muda tena kama ilivyo katika Aya hii na nyinginezo.

Na ijapokuwa baadhi yao hawakuapa kuwa hapana Kiama—lakini kule kutoushughulikia uhai wa huko ni kama alama kuwa hawauamini uhai huo. Kama kweli wanauamini kwa nini wasiushughulikia!

45. “Na mkakaa katika mahala mle mle walimokuwa wakikaa wale waliodhulumu nafsi zao, na ikakudhihirikieni jinsi tulivyowafanya: na tumekuelezeni mithali (zote; na nyinyi hamkujali kitu).”

46. Na kwa hakika walifanya hila zao, na hila zao ziko kwa Mwenyezi Mungu (anazijua). Wala haiwi hila zao kuweza kuondosha majabali; (yaani haziwezi hila zao kuondosha yaliyothubutu).

47. Basi usimdhania Mwenyezi Mungu kuwa mwenye kuwavunjia ahadi yake Mitume yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda na ndiye Mwenye kulipiza.

48. (Ikumbukeni) siku ambayo ardhi hii itabadilishwa kuwa ardhi nyingine, na mbingu (pia ziwe namna nyingine); nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu, mmoja (peke yake), Mwenye nguvu (za mwisho).

49. Na utawaona wakosa siku hiyo wamefungwa katika minyororo.

50. Nguo zao zitakuwa za lami, na Moto utazijia nyuso zao (uzibabue)

51. Ili Mwenyezi Mungu ailipe kila nafsi kwa yale iliyoyachuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

52. Haya yatosha (kuwa mauidha) kwa watu, ili waonywe kwayo, na wapate kujua kuwa Yeye (Mwenyezi Mungu) ni Mungu Mmoja tu, na ili wenye akili wakumbuke.

وَسَكَنَتْهُمْ فِي مَسْكِنٍ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ
وَتَبَيَّنَ لَكُمْ كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا
لَكُمْ الْأَمْثَالَ ۝٤٥

وَقَدْ مَكَرُوا مَكْرَهُمْ وَعِنْدَ اللَّهِ مَكْرُهُمْ
وَإِنْ كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ ۝٤٦

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُخَلَّفًا وَعِدَةٍ رَسُولُهُ إِنَّ اللَّهَ
عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ۝٤٧

يَوْمَ تَبْدُلُ الْأَرْضَ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتِ
وَبَرَزُوا لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ۝٤٨

وَتَرَى الْمَجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُّقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ۝٤٩

سَرَابِيلُهُمْ مِنْ قَطَرَانٍ وَتَعْشَى وُجُوهُهُمْ النَّارُ ۝٥٠

لِيَجْزِيَ اللَّهُ كُلَّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ
إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ۝٥١

هَذَا بَلَاغٌ لِلنَّاسِ وَلِيُنذَرُوا بِهِ وَيَعْلَمُوا أَنَّمَا

هُوَ إِلَهُ وَاحِدٌ وَلِيَذَّكَّرُوا أَلْوَا الْأَلْبَابِ ۝٥٢

48. Wameyasopotoasopotoa maelezo ya Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 49 ili watimize ule ukafiri wao — walioutia katika Aya ya 24 waliyoifanya ni ya 25 ya *Suratul Baqarah*—na kusema kuwa maisha ya Akhera hayatakuwa ya kiwiliwili. Yatakuwa ya kiroho tu. Tazama jawabu ya Uislamu katika maelezo yetu juu ya Aya hizo katika *Suratul Baqarah*.

52. Tumepewa akili tuitabiri (tuzingatie); ikiwa hatuzingatii tutakuwa kama wanyama. Basi sisi ndio tutakaokuwa na lawama. Wao hawajapewa hiyo akili.